

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA



Kumb.Na:KDC/L.40/10/44

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha imepokea kibali cha ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2021/2022 chenye Kumb. Na. FA.97/228/01/9 cha tarehe 13 Mei, 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kupitia kibali hicho, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Kibaha anapenda kuwatangazia wananchi wote kuomba nafasi hizo kama zilizoorodheshwa hapa chini.

1. KATIBU MUHTASI DARAJA LA III (PERSONAL SECRETARY III). *NAFASI TATU*
(03)

(a) SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu na **kufaulu** kidato cha nne au sita na aliyehitimu kozi ya Uhazili na **kufaulu** mtihani wa Hatua ya Tatu.
- Aliyefaulu somo la Hatimkato la Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- Awe amesoma mafunzo ya *Kompyuta* kutoka chuo chochote kinachotambulika na Serikali, na kupata cheti katika programu za *Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail* na *Publisher*.

(b) KAZI NA MAJUKUMU YA KATIBU MUHTASI DARAJA LA III

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwaelekeza sehemu sahihi
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi na kumtaarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika
- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika kwa shughuli za kiofisi.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maafisa walio katika sehemu alipo. Kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu husika.
- Kutekeleza majukumu mengine atakayokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

Mshahara: Ngazi ya mishahara ya Serikali ya **TGS B1** kwa mwezi.


MASHARTI YA JUMLA:

- Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
- Awe raia wa Tanzania
- Aambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu zilizosajiliwa kwa majina yake kamili, ikiwa ni pamoja na wadhamini wawili na anuani zao kamili.
- Awe na Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- Aambatanishe picha mbili "Passport size" za hivi karibuni na kuandika majina yake.

- Watakaofaulu kuitwa kwenye usaili, majina yao yatawekwa kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya Kibaha yaani: www.kibahadc.go.tz
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 06 Juni 2022 saa 9:30 Alasiri

Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 30153
KIBAHA.


B.N. Ndalahwa
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KIBAHA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KIBAHA

Nakala: - Katibu
Ofisi ya Rais
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma
S.L.P 2320
DODOMA.